Matokeo ya utafiti wa mradi wa Minara ya Maji, Itare, Msitu wa Mau

Lengo:

Kutambua iwapo na ni kwa njia gani vyama vya msitu wa jamii na jumuiya za watumiaji rasilimali zinashirikiana katika kusimamia rasilimali za msitu na maji

Douglas Bwire, Esther Mwangi, Sylvia Rotich

Maelezo ya jumla ya msitu wa Itare

Msitu wa Itare unapatikana kusini-magharibi mwa msitu wa Mau, na una eneo la jumla ya hekta 16,700. Chama cha msitu wa jamii (CFA) cha Itare, ambacho kina wanachama wapatao 2000, kina makundi ya watumiaji wafuatayo: wafugaji nyuki, wachungaji mifugo, wavunaji maji, utalii wa ikolojia, wakusanyaji kuni, wavuvi, vitalu vya miti, wafugaji vipepeo, wazalishaji wa uyoga na wachimbaji mawe. Jumuiya ya watumiaji wa rasilimali ya maji (WRUA) ya Chemosit, ambayo ina wanachama 72, inapatikana katika bonde ndogo ya Itare-Chemosit (eneo la kilomita za mraba 247). Wanajamii 32 ni wanachama wa CFA na wa WRUA. Wengi wao ni wanaume wa umri wa miaka 35 au zaidi, kama Kielelezo 1 kinaonyesha.

Mchakato wa utafiti

Vyama viwili vya kijamii (CBO) vya Kaptebengwet na Cheptalal vilichaguliwa. Makundi ya watumiaji yafuatayo yalichaguliwa: wakulima, wasimamizi wa maji, vitalu vya miti, wafugaji nyuki na wakusanyaji kuni. Tulifanya majadiliano na vikundi 30 tukijumuisha wanachama na wasio wanachama wa CFA na WRUA, na mijadala ya vikundi maalum (focus group discussions) 6 na viongozi. Tulijadiliana na wanaume na wanawake 247 kwa jumla ambao walitenganishwa kwa umri kama inavyoonyeshwa kwenye Kielelezo 1.



Kielelezo 1. Usambazaji kwa jinsia wa wanachama wa CFA na WRUA.

Kielelezo 2. Asilimia ya washiriki wanawake na wanaume katika majadiliano ya vikundi maalum.

Kielelezo 3. Idadi ya mijadala ya vikundi maalum kwa kila kikundi cha watumiaji Itare

Mtazamo wa jamii wa hali na mabadiliko ya msitu na maji

Katika kipindi cha miaka 5 hadi 10 iliyopita, wastani wa eneo la msitu ulipungua na spishi za miti ya asili kama mvule na lemongrass (awonet, rerendet) imekwisha toweka. Baadhi ya sababu za mabadiliko haya ni ongezeko la idadi ya watu, shughuli zisizo halali kwa mfano ufugaji wa kupita kiasi na uchomaji mkaa, na mahitaji ya nishati ya kuni kwa viwanda vya chai.

Mito midogo kadhaa pia imekauka kabisa katika kipindi hiki (Itare-Chemosit, Kipsanai). Mafuriko yamesababisha mchangotope. Sababu za kukauka mito na kuongezeka kwa mchangtope ni pamoja na utoaji zaidi wa maji kwa watumiaji walio sehemu za juu za mto, kilimo duni kwenye miteremko ya milima na kando ya mito, na upandaji miti ya mkaratusi karibu na vyanzo vya maji.

Kiungo kati ya msitu na maji: Wanajamii wanao uelewa wa uhusiano wa mabadiliko ya misitu na viwango na ubora wa maji. Katika mijadala ya vikundi maalum 29, washiriki walitaja upunguaji wa mwavuli wa msitu kama sababu ya viwango vya maji kupungua na vijito kukauka. Miungoni mwa washiriki hawa, wanawake vijana walikuwa na mtazamo tofauti. Kwa mujibu wao maji ni masafi kwa sababu wanajamii wamejitahidi kikamilifu kuihifadhi rasilimali hiyo. Wazee wakiume na wakike nao wakasema vijito vilikauka kwa sababu ya ukataji miti wakiongeza kuwa upandaji miti ya mkaratusi pia umechangia ukaukaji wa vijito. Kilimo kwenye miteremko ya milima husababisha mmomonyoko wa udongo na miti ya mkaratusi kwenye kinga za mito yalitajwa kuwa baadhi ya sababu za uchafuzi na kubadilika rangi kahawia kwa mito.

Uongozi

Mwenyekiti na katibu wa CFA ni wanaume, na mweka hazina ni mwanamke. Katika ngazi ya vikundi vya watumiaji, waweka hazina wote ni wanawake. Vikundi tatu pekee (Tomboiyot, Arise and Shine, na Mt. Sinai) kati ya kumi vilichagua wanawake kama mwenyekiti. Kipindi kwa ofisi katika CFA ni miaka mitatu na uchaguzi wa mwisho

ulifanyika mwaka wa 2016. Wanawake huchaguliwa kwa sababu wanaonekana kuwa wanajitimu na niwakuaminika. Wanaume huchaguliwa kwa sababu mila za kitamaduni zinahusisha wanaume na nafasi za uongozi wa juu. Kwa kuongeza, wanaume hawajishuilishi na kazi za nyumbani

WRUA ina ngazi mbili za uongozi: menejimenti na kamati ndogo nne za ununuaji, usimamizi wa mafuriko na ukame, ufuatiliaji, shughuli za maisha na fedha. Ngazi ya menejimenti ina wanaume wanne na mwanamke mmoja. Ngazi ya kamati ndogo ina wanawake 15 na wanaume 15. Kipindi kwa ofisi katika WRUA ni miaka mitatu na uchaguzi wa mwisho ulifanyika Juni 2018.

Shughuli kwa pamoja kati ya CFA na WRUA

Wengi wa wanachama wa CFA hawakuwa na shughuli kwa pamoja na wenzao wa WRUA. Vikundi vya watumiaji 4 kati ya 10 walisema walishirikiana na WRUA. Ingawa baadhi ya wanachama walikiwa katika vikundi vya CFA na pia wanachama wa WRUA na wakawa na shughuli kwa pamoja, haijulikani kwa wazi ni shughuli gani zilitendeka kwa pamoja na ni kwa muda gani. Wanachama wa CFA walitaja uanzishwaji wa vitalu vya miti kama shughuli kwa pamoja, na wanachama wa WRUA wakataja ushirikiano kwa ukataji miti ya spishi za mkaratusi kwenye kinga za mito, na ufugaji nyuki.

Jedwali la 1 Wanachama wa vikundi vya watumiaji vya CFA walio pia wanachama wa WRUA.

Kikundi cha watumiaji (CFA)	Wanachama	Wanachama wa WRUA
Arise and Shine (Ufugaji mifugo)	Wanaume na wanawake wazee	7 kati ya 13
Meswondo (Ukusanyaji kuni)	Wanaume na wanawake wazee	5 kati ya 11
Kapleleito (Vitalu vya miti)	Wanawake vijana	3 kati ya 14
Sakweta (Utoaji maji)	Wanawake wazee	9 kati ya 20
Kiptobon (Ufugaji nyuki)	Wanawake wazee	1 kati ya 60

Shughuli za vikundi vya watumiaji vya CFA zilihusisha maeneo ya msitu pekee na hakuna kundi lililohusika na usimamizi wa maji. Vile vile, wanachama wa WRUA hawakujihusisha na usimamizi wa msitu na badala yake walipendelea maeneo kando kando ya mito na vijito (riparian areas). Shughuli zilikuwa za kupanda miti ya asili kwenye kingo za mito na kupanda mianzi ili kuondoa miti ya mkaratusi kwenye kingo za mito ya Kisumeki na Itare Chemosit. Sababu zilizotolewa za kukosa shughuli kwa pamoja zinajumuisha ukosefu wa ujuzi wa kutosha kuhusu shughuli za WRUA na CFA, na kutoridhika na uongozi.

Shughuli ya kwanza kwa pamoja ya CFA na WRUA ilitokea baada ya kuanzishwa kwa programu hii ya utafiti wa Minara ya Maji. Ilihusisha upandaji miti ya asili 5000 katika eneo la Kabaibai mwezi Julai 2018. Aina za spishi zilizopandwa ni *lamaiywet, arorwet, rerendet, silipchet* na mianzi.

Ushiriki wa wanachama wa CFA na WRUA kwa mikutano

Ushiriki wa wanawake ulikuwa dhaifu na baadhi ya changamoto zilizowakumba ni ukosefu wa muda kutokana na kazi za nyumbani na umbali wa kufikia mikutano. Hakukuwa na mikutano kwa pamoja kati ya CFA na WRUA.

Mapendekezo ya kuboresha ushirikiano

Viongozi wa CFA na WRUA wanatakiwa kuandaa mikutano ya wanachama wao katika maeneo yanayo fikiwa kwa urahisi, na kutoa taarifa awali za siku, tarehe, na mahala pa mkutano. Wanaweza pia kutoa msaada wa kifedha kwa wanachama ili walipie nauli ya kusafiri kufikia mikutano.

Shughuli zilizopendekezwa za ushirikiano kati CFA na WRUA

- Uanzishwaji wa vitalu vya miti, usimamizi wa kinga za mito
- Ushirikiano katika shughuli za kuzalisha mapato k.m. maji ya chupa, ufugaji nyuki.

La kushangaza ni kwamba mikutano kwa pamoja ya CFA na WRUA haikuwa sehemu ya shughuli zilizo-pendekezwa.

Hitimisho

Wanachama wa CFA na WRUA wanao uelewa wa uhusiano uliopo kati ya misitu na maji. Walieleza kuwa mabadiliko ya viwango na rangi ya maji yanahusiana na uharibifu wa misitu. Hata hivyo, shughuli kwa pamoja hazipo nyingi, hata katika zile nyakati chache ambako uanachama uliingiana. Uongozi wa CFA na wa WRUA ulijumuisha hasa wanaume, na wanawake wakachukua jukumu la mweka hazina. Shughuli za WRUA na CFA zilihusisha hifadhi za maeneo kando ya mito kwa WRUA na uhifadhi wa misitu kwa CFA. Wanachama wa WRUA na wa CFA walikubaliana kufanya kazi kwa pamoja katika shughuli kadhaa. Shughuli kwa pamoja za upandaji miti, kuanzisha vitalu vya miti na uhifadhi wa maeneo kando ya mito na vijito zilitajwa kuwa na uwezekano wa kushirikiana.

Mapendekezo

- Kuimarisha ushirikiano kati ya Itare CFA na Itare-Chemosit WRUA.
- Kuongeza ufahamu ili wanachama wa CFA waanzishe shughuli za usimamiaji maji katika sehemu za chini, na wanachama wa WRUA watekeleza shughuli za usimamiaji msitu.
- Kutoa mafunzo maalum ya kujenga uwezo ili kuimarisha uratibu kati ya CFA na WRUA na kuimarisha ushiriki wa wanawake kuwania nafasi za menejimenti katika vyama hivi viwili.

Kuandaa mikutano ya pamoja kati ya uongozi wa CFA na WRUA kama hatua ya kwanza ya kufikia ushirikiano.

Na ufadhili wa

Federal Ministry for Economic Cooperation and Development

Lancaster University

KENYA Forest Service

the green belt movement